## **Kurunzi Za Mitandao**

*Na Anthony Mwaikwasi*

Mitandao ya kijamii ndio yangu azizi
Huku nashea maclip na kueka mambo wazi
Kuchapisha siasa na uvumi fesibuku ndio kazi
Posti zote si akili zangu bali zingine ni za wizi
Si wizi wa kukaba bali kufoward bila uchunguzi

Je ninavyofanya ni sawa au haki
Akili yanisuta na nafsi kunishtaki
Ila sikomi maana kwa mablog mimi shabiki
Sina muda wa kuchunguza kama kweli au mikiki
Kichelewesha kuposti ladha takwisha na takosa kiki

Otieno na Lucy juzi kaniita na kunipa kali kisomo
Yangu tabia ya kuposti bila kuhakikisha ukweli ifike kikomo
Maana habari za kizushi na uongo zimejaa mpaka pomo
Nayo serikali imeeka makachero kuchunguza wenye mdomo
Watakushika kupitia OSINT hata ukiamua kujificha bara Pokomo

Kabla ya kurusha mambo mtandaoni piga kurunzi
Kuhakikisha unayoyasema na kushea yana mzizi
Wa kweli na sio uchonganishi wa hadhira waziwazi
Sababu kishikwa na hatia tapata mapya makazi
Sio kwenye orofa za nyali bali jela ndio takuwa malazi

***© 2025 [Anthony Mwaikwasi Kimbio]***